

### Taarifa Kwa Vyombo vya Habari

## **Polisi Nchini Tanzania Wamepiga Marufuku Kongamano la Hizb ut Tahrir la Kuikaribisha Ramadhan**

Polisi kwa kiburi wamepiga marufuku kongamano la Hizb ut Tahrir la kuikaribisha Ramadhan ambalo ilikuwa lifanyike mnamo Jumamosi 20 Mei 2017 katika Hoteli ya Mayfair, jijini Dar es Salaam. Polisi walitoa barua ya vitisho kwa hoteli hiyo iliyo andikwa tarehe 19 Mei 2017 ambapo ilikuwa imebakia saa chache tu kabla ya kuanza kwa kongamano hilo. Kisingizio nyuma ya kupigwa marufuku huku kilikuwa ni kwamba kongamano hilo lilitolewa siku moja kabla ya kongamano hilo na kutuarifu sisi saa chache tu kabla ya hafla hiyo?

Sisi katika Hizb ut Tahrir tunashangaa, je, kweli mkutano wa siri unaweza kufanyika katika eneo la hotel ambalo linabeba zaidi ya waalikwa 450? Au je, mkutano wa siri kweli utaalika hadharani watu maarufu kadha wa kadha, ikiwemo masheikh, maimamu, wasomi, wanasiasa, waandishi wa habari, mawakili, wanaharakati, nk? Ikiwa hiyo ndio sababu, ni kwa nini barua ya kupiga marufuku kongamano hilo ilitolewa siku moja kabla ya kongamano hilo na kutuarifu sisi saa chache tu kabla ya hafla hiyo?

Kadhia hii pia inafichua udhalimu na ukandamizaji wa nidhamu ya kidemokrasia, kama inavyo dhihirishwa na serikali zake kote ulimwenguni, ambapo zinadai kuenzi ule unaoitwa uhuru wa kuabudu na kujieleza huku kiuhalsia ikiwa ni miito mitupu tu.

Kwa unyenyekevu mkubwa, tunatoa samahani kwa waalikwa wote kutokana na uzito wowote ambaao huenda waliupata kutokana na kupigwa marufuku hafla hii muhimu iliyo lenga kugusia kadhia nyeti ikiwemo kufeli kwa nidhamu ya kirasilimali duniani. Vilevile, tunawakumbusha kwa unyenyekevu kuwa hali hii ni ishara waziwazi ya kushindwa, kutofaa na kutostahiki kwa urasilimali na nidhamu yake ya kisiasa ya demokrasia iliyo mnyima mwanadamu kila kitu ikiwemo fursa ya kufanya majadiliano juu ya kadhia nyeti. Wakati uwewadia kwa kila mwenye kutafakari kwa undani kutafiti mfumo mbadala ambaao bila shaka ni Uislamu na nidhamu yake ya utawala ya Khilafah.

**Masoud Msellel**  
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania**